

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Simu: +255-26-2323189

Barua pepe: ps@moha.go.tz

Tovuti: www.moha.go.tz



PSPF Dodoma Plaza,
Ghorofa ya 11,
Barabara ya Benjamini Mkapa,
S. L. P. 2916,
40483 DODOMA.

06 Julai, 2019

**TAASISI ZA KIDINI NA JUMUIYA ZA KIJAMII KATIKA
MIKOA YA MBEYA, IRINGA, NJOMBE, RUKWA NA SONGWE
KUHAKIKIWA KUENZIA TAREHE 15 JULAI, 2019 HADI 24
JULAI, 2019**

Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kijamii na Taasisi za Kidini, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, itaendesha awamu ya tatu ya zoezi la uhakiki wa Taasisi za Kidini na Jumuiya za Kijamii katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Rukwa na Songwe kuanzia tarehe 15 Julai, 2019 hadi 24 Julai, 2019.

Zoezi la Uhakiki litafanyika katika Kituo cha Uhakiki kitachokuwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

Wakati wa uhakiki kila Taasisi itatakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-

1. Cheti halisi cha usajili na kivuli cha cheti hicho.

2. Stakabaadhi ya malipo ya ada ya hivi karibuni.
3. Katiba ya Jumuiya/Taasisi husika iliyopitishwa na Msajili.
4. Barua inayothibitisha uwepo wa Jumuiya/Taasisi hiyo toka kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kata mahali ilipo Ofisi ya Jumuiya/Taasisi husika.

Fomu ya Uhakiki inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa anuani www.moha.go.tz na kwenye Kituo cha Uhakiki.

Taasisi ambazo zitashindwa kuhakikiwa kwa mujibu wa ratiba ya eneo husika zitalazimika kwenda Makao Makuu ya Wizara Dodoma kwa ajili ya uhakiki na iwapo zitashindwa kufanyiwa uhakiki kwa muda uliopangwa zitaondolewa kwenye orodha ya Msajili.

Aidha kwa Taasisi za Dini na Jumuiya za Kijamii ambazo hazijasajiliwa zitatakiwa kufika wakati wa zoezi la uhakiki kwa ajili ya kupewa utaratibu wa kupata usajili.

Malipo ya ada yatafanyika wakati wa zoezi la uhakiki kupitia mfumo wa malipo ya Serikali kwa njia ya Kielektroniki (Government Electronic payment Gateway System).

Imetolewa na:


Meja Jenerali Jacob G. Kingu, *ndc*

KATIBU MKUU